# *Napenda sana sheria yako*

*ZABURI 118*

*Composé par: Gloire VINCENT*




1. Nimesema, ee Bwana, sehemu yangu
nikushika maneno yako.
Sheria ya kinywa chako imenifaa zaidi
kuliko maelfu ya zahabu na feza.

2. Wema wako unitulize kwa neno,
ulilomwambia mtumishi wako.
Rehema zako zinifikie nipate kuishi,
kwani sheria yako ni furaha yangu.

3. Kwa hiyo ninapenda maagizo yako
kuliko zahabu, hata zahabu safi.
Kwa hiyo nimeelekea amri zako zote,
nimechukia kila njia ya uwongo.

4. Mafundisho yako ni ajabu,
ndiyo maana roho yangu inayashika.
Ufunuo wa maneno yako unaangaza,
unawaelimisha wale wasiojua.